***Learning by Ear –Elimu na Kazi***

**Elimu ya Chuo Kikuu**

**Hadithi ya Malaika / Episode 2**

**Mwandishi: NJOKI C. Muhoho**

**Mhariri: Maja Dreyer**

**Tafsiri: Eric Ponda**

---

*WAHUSIKA:*

Mtangazaji Mwanamume

Malaika Miaka 19, Msichana

Bi Grace: Miaka 52, Mwalimu wa zamani wa Malaika

Daniel: Miaka 20, mwanafunzi wa mwaka wa pili katika kitivo cha Malaika

Cindy: Miaka 19, mkazi mwenza katika chumba cha Malaika chuoni,kutoka familia tajiri.

---

**INTRO**

**MUZIKI**

## 1. Mtangazaji:

Hujambo na karibu kwa awamu ya pili ya "Learn By Ear", Ukiwa ni mfululizo wa vipindi vyetu tukinaangazia masuala ya elimu na Kazi. Katika makala yetu ya mwisho, Malaika kwa usaidizi wa Mwalimu wake na

shangaziye wafanikiwa kuishawishi familia yake kuhusu umuhimu wa kujiunge na chuo kikuu. Na kutokana na msaada wa wanakijiji na pia kupitia mikopo, ndoto hiyo sasa inatimia. Leo hii, mnasihi wake ambaye ni mwalimu wake wa zamani Bi Grace, ana msindikiza hadi jijini kujiunga na chuo hicho kikuu.

## Scene 1: Kituo cha Mabasi Jijini

**SFX:** ***MAKELELE YA KITUO CHA MABASI, MUZIKI,HONI ZA MAGARI, WAHUDUMU WA MABASI WAKIWAITA ABIRIA NA SAUTI ZA MAGARI MADOGO.***

2. MALAIKA — ***(akiwa na wasi wasi)*** Mwalimu Grace, hapa kuna makelele na pia kutatanisha.

3. MS GRACE — Ndio, lakini usikubali kuhangaishwa na mtu yoyote. Hili ni jiji sio kule mashambani..

4. MALAIKA — Sawa mwalimu!

5. MS GRACE — Hapa jijini kila mmoja anafuata shughuli zake, usikubali kabisa kuhangaishwa na mtu yeyote. Wewe.. ushikilie mkoba wako kikiki, ama sivyo utapokonya sasa hivi.

6. MALAIKA: — Ndio mwalimu. Bi Grace, naogopaa!

| | |
|---|---|
| 7. Bi GRACE | Ningeshikwa na wasiwasi zaidi kama hungekuwa unajali au kuogopa. Funzo la kwanza,.. lazima uwe kifua mbele, usiwe kama kuku aliyenyeshewa.. hawa watu watakupora sasa hivi ukizubaa! Ni lazima uonyeshe ujasiri kwamba pia wewe umo! ***(akimuita mpita nji)*** wewe… ehh wewe!.. Njia ya kuelekea chuo kikuu ni ipi? |
| 8.MAILAIKA | Lakini mwalimu Grace, si unasema unajua mahali kilipo chuo kikuu? |
| 9. Bi GRACE | Funzo la pili. Iwapo ni lazima utafute msaada kutoka kwa mpita njia, basi usionekane kama wewe ni zuzu, la sivyo watatumia fursa hiyo kukutenda. |
| 10. MALAIKA | ***(akimtania)*** Ahh, mafunzo tena, nilifikiri wewe si mwalimu wangu tena! |
| 11. Mtangazaji | Wakiwa wamebeba sanduku zito na mikoba, Malaika na Mwalimu Grace wanakaribia lango la chuo kikuu. |

**MUZIKI.**

## SCENE 2: LANGO LA CHUO KIKUU

SFX: ***Hali ya ukimya, isipokuwa tu sauti za jiji kwa mbali. Ndege wakiimba.***

| | |
|---|---|
| 12. Bi GRACE | Ohoo, hebu tizama lango la chuo kikuu. Hatimaye msichana wangu! Sasa wapi ofisi ya msajili mkuu? |

SFX: ***Sauti za nyayo zikikaribia*.**

| | |
|---|---|
| 13. DANIEL | Habari zenu. Mnahitaji msaada wowote niwasaidie? |
| 14. MALAIKA | Ndio. |
| 15. Bi GRACE | *(**akimkatiza** )* Hebu kidogo mvulana, na wewe ni nani? |
| 16. DANIEL | Naitwa Daniel, mimi ni mwanafunzi hapa. (***akimgeukia Malaika****)*, nikusaidie kubeba sanduku hili . |
| 17. Bi GRACE | Uuuh….Mbona usinisaidie mimi…….? |
| 18. **Mtangazaji.** | Wakiandamana na mwanafunzi huyo, wawili hao wanafululiza moja kwa moja hadi ofisi ya msajili chuoni. Ingawa kuna alama za kuwaelekeza wageni chuoni humo, ni rahisi mtu kupotea hata kama anaye muelekezi. Malaika anajaza fomu za usajili bila matatizo na kukabithiwa |

kitambulisho cha uanafunzi, na funguo za chumba cha bweni atakamoishi chuoni humo. Inayosalia sasa ni kutafuta kiliko chumba hicho.

SFX: ***Muziki wa sauti ya juu na makelele yasikika kwa mbali.***

19.Bi GRACE Kwani kuna disco mahali hapa? Huo muziki ni wa sauti ya juu sana.

20. MALAIKA Oooh… hiki chumba changu hapa!

21. Bi GRACE Enzi zetu tulikuwa tukisoma kwa ukimya, sio fujo na makelele kama haya.

SFX***: Abisha huku muziki ukisikika chumbani. Mlango wafunguliwa na sauti ya muziki yaongezeka.***

22. CINDY ***(sauti yaongezeka)*** Habari zenu!

23. MALAIKA Nzuri. Mimi naitwa Malaika mkaazi mwenza wa chumba hiki.

24. CINDY Naitwa Cindy. Kwa hiyo wewe ni mwenza hapa chumbani! Basi karibu ndani!

25 Bi GRACE Malaika sasa nadhani naweza kuwaacha ili nipate usafiri wa kurejea kijijini kabla giza kuingia. Kwa heri na kila la kheri!

26. MALAIKA Akhsante sana Mwalimu Grace, wasalimie wazazi ukifika.

SFX***: Hatua zikitokomea, sauti ya sanduku likiburutwa sakafuni***.

27. CINDY — Oooh ulilipata wapi …hilo boksi..hilo sanduku?,… kutoka kwa makavazi ya kitaifa?

28. MALAIKA — Oooh hili….. napendelea sana haya kuliko yale makubwa.

29. CINDY — Nini? Ooh pole…?

30. MALAIKA — Ni hadhithi ndefu tu!

31. CINDY — Naona nina kibarua cha kukufunza hapa.

32.**Mtangazaji** — Malaika ameachana na mshauri wake, Mwalimu Grace, lakini inavyoonekana ni kana kwamba amempata mshauri mpya. Na Ili kumudu maisha ya Jiji, anahitaji sana usaidizi wa Cindy. Lakini je kimasomo itakuwaje?

**Muziki**

## <u>Scene 3: Chumbani mwa Cindy/ Malaika</u>

**SFX: *Makelele ya usiku huku mtu akikoroma taratibu. Mlango wafunguliwa kwa fujo..***

33. CINDY — ***(Aamka kwa uvivu)*** Malaika, ni wewe?

34. MALAIKA — ***(kwa unyenyekevu)*** Pole.. nimekuamsha?

35. CINDY — Ni saa ngapi?

36. MALAIKA — Najisikia mchomvu …..na njaa pia!.

37. CINDY — Usiniambie mwenzangu watoka darasani kusoma saa hii. Si utajiuua.!

38. MALAIKA — (***mwenye huzuni***) Masomo ni magumu, nina kazi nyingi na sitaki kuanguka mtihani, kwani nawajibika sana kijiji mwangu.

39. CINDY — (***akiwa ameudhika***) Sawa, tosha tosha! nimesikia mengi tu kuhusu hicho kijiji chako!.... kwamba kijiji changu kina hivi, kijiji changu kina vile, kwani hao wanakijiji walikwambia usiponde raha? Uhh unaudhi!

40. MALAIKA — Kwako wewe ni rahisi kwa sababu babako ni tajiri.

41. CINDY — *(**ameudhika**)* Sikia wewe msomi, mimi ni msichana kama wewe. Pia nawajibika kwa babangu, ndugu zangu na ulimwengu mzima, lakini sio kila saa ni kitabu tu mchana kutwa, usiku kucha, kisha uje kumuamusha mwenzako usiku wa manane. Unahitaji kupumzika. Haya tulale basi kesho nitakufunza mawili matatu jinsi ya kuishi maisha ya chuo kikuu! Usiku mwema au tuseme kumekucha?

42. **Mtangazaji** Kwa unyonge na mwenye kuchanganyikiwa Malaika apanda kitandani. Hana hakika iwapo atawezana na maisha ya Cindy. Alala akiwawaza.

***<u>SCENE 4: KWA BAA AU UKUMBI WA DISCO.</u>***

**SFX: *MUZIKI WA DISCO NA MAKELELE***

43. *MALAIKA*: *(**Amesisimka**)* Ilikuwa filamu nzuri.

44. CINDY: *(**akikokoteza**)* Nitakunywa hii… Kunywa …kunywa hiyo…!

45. MALAIKA: *(**akikokoteza**)* Ni kali, kwa nini unakunywa?

46. CINDY *(akimtania )* Kujiburudisha! Baada ya masomo

mchana kutwa, nahitaji kujiliwaza kidogo angalau kupumzisha akili. Lakini sisemi uwe mlevi.

47. MALAIKA: Uhhh huu….. sipendi kunywa pombe.!

48. CINDY: Sawa basi, sasa tunasubiri nini, tuingie uwanjani tucheze.

**SFX: Kicheko na Muziki, huku wasichana hao wakiingia uwanjani kucheza. Sauti ya ukumbi wa muziki ikitoweka.**

**Muziki**

***SCENE 5: MALAIKA/ CINDY CHUMBANI***

SFX: ***Kengele ya saa yalia kisha kunyamaza, yalia tena na kunyamaza***

49. CINDY — Malaika, amka.. amka sasa !

50. MALAIKA — (***akijisikia mvivu***) Aaah, wacha nilale….. niache…!

51. CINDY — Amka …..umesahau una mtihani?..

52. MALAIKA — (***usingizi wamtoka***) Ooh hapana…… siko tayari!

**MUZIKI**

**OUTRO**

**53. MTANGAZAJI**

Malaika sasa umegundua kuna raha katika maisha ya chuo kikuu.Na zaidi, yapo mengi ya kujifunzo maishani mbali na vitabu.Lakini mbali na hayo pia anafahamu barabara wajibu wake kimasomo. Amewapata marafiki wengi kama ilivyo kwa mwenzake Cindy. Lakini Je marafiki hawa watamsaidia kumtoa Malaika kwenye njia panda?

Ungana nasi kwa kipindi kijacho cha “Learning By Ear, Noa Bongo jenga maisha yako” kuhusu maisha na elimu ya Chuo Kikuu. Pia unaweza kutusikiliza kupitia mtandao wetu www.dw-world.de/lbe ujifunze mengi kuhusu vipindi hivi. Ukiwa na maoni unaweza pia kututumia. Hadi wakati mwengine, Kwa heri kwa sasa.